




# UTAFITI WA AFYA YA UZAZI NA MTOTO NA VIASHIRIA VYA MALARIA TANZANIA

## TDHS/MIS 2021-22



# TDHS/MIS 2021/22 Yaliyomo



1

## Utangulizi

- Madhumuni
- Historia
- Kamati za Utafiti

2

## Utekelezaji wa Utafiti (TDHS/MIS 2021-22)

- Sampuli
- Mafunzo na Zoezi Halisi la Kuorodhesha Kaya
- Mafunzo na Utafiti wa Majaribio

3

## Hatua zinatofuata za Utekelezaji wa Utafiti

- Mafunzo na Ukusanyaji wa Taarifa za Utafiti
- Kuandaa Ripoti ya Utafiti
- Usambazaji wa Matokeo ya Utafiti





## UTANGULIZI

**Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria umekuwa ukifanyika kila baada ya miaka 5.**

**Mara ya mwisho Utafiti wa namna hii ulifanyika nchini mwaka 2015-16.**



**Viashiria vinavyotokana na Utafiti huu vinasaidia kutambua hatua tuliyofikia katika sekta ya afya ili kuweza kupanga mipango mbalimbali ya kitaifa na kimataifa pamoja na jamii kwa ujumla.**

**Utafiti wa TDHS/MIS 2021-22 unakusanya takwimu katika ngazi ya kaya kwa dhumuni la kuwezesha upatikanaji wa takwimu sahihi na zenye ubora kuhusiana na taarifa za msingi za kaya na jamii.**

**Ikumbukwe kwamba taarifa zote za wanakaya zitabaki kuwa ni SIRI kati ya mdadisi na mhojiwa. Nyenzo zote za utafiti huu zinatunzwa kwa uangalifu mkubwa na hazitaoneshwa kwa mtu yeyote asiyehusika na Utafiti huu.**

# HISTORIA YA UTAFITI


Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2021-22 (2021-22 TDHS/MIS) ambao utafanyika kuanzia Februari 2022, utakuwa ni wa 6 kufanyika nchini.

Tafiti nyingine za TDHS zilizofanyika nchini ni pamoja na;




**1991-92**

Tanzania




**1996**

Tanzania




**2004-05**

Tanzania




**2009-10**

Tanzania



**2015-16**

Tanzania





# Kamati za Utafiti

## Kamati ya Ushauri

- Kupitisha nyaraka zote za Utafiti na kuidhinisha masuala yote ya kitaalam yanayohusu Utafiti
- Kuhakikisha rasilimali fedha zinapatikana
- Kuhamasisha serikali ya Tanzania kupata na kutumia takwimu katika mipango ya maendeleo na utungaji wa sera

**Mwenyekiti: MOHCDGEC**

### Wajumbe

NBS, OCGS, MOHCDGEC-Mainland&Zanzibar, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tamisemi, Taasisi ya chakula na lishe, Mpango wa Kitaifa-TFNC wa Kuthibiti Malaria-NMCP, USAID, UNICEF, CDC, ICF, Nutrition International, Royal Norwegian Embassy, WHO, DFID, GIZ, UDSM, SUA, UDOM

## Kamati wa Wataalam

- Kuboresha moduli zilizowekwa kwenye madodoso
- Kupitia na kushauri sampuli ya utafiti
- Kuhakikisha taratibu za kufanya Tafiti za kitabibu zinafuatwa
- Kuratibu maandalizi ya ukusanyaji wa taarifa ikijumuisha kutoa taarifa za utendaji kwa kamti ya wadau
- Kuandaa ripoti ya matokeo muhimu na ripoti kuu
- Kutoa matokeo ya Utafiti kwa wadau

**Mwenyekiti: SG/OCGS**

### Wajumbe

NBS, OCGS, MOHCDGEC-Mainland & Zanzibar, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tamisemi, Taasisi ya chakula na lishe, Mpango wa Kitaifa-TFNC wa Kuthibiti Malaria-NMCP, USAI, UNICEF, CDC, ICF, Nutrition International, Royal Norwegian Embassy, DFID, GIZ, UDSM, SUA, UDOM, WFP, LHRC, GOT, Global Affairs Canada, United Kingdom FCDO, Irish Aid, German (KFW/GIZ), PSI

## Kamati ya Wadau

- Kupitia na kuridhia maswali yaliyowekwa kwenye madodoso ya Utafiti
- Kupendekeza maswali na moduli mpya ili ziingie kwenye utafiti

**Mwenyekiti: MOHCDGEC**

### Wajumbe

NBS, OCGS, MOHCDGEC-Mainland&Zanzibar, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tamisemi, Taasisi ya chakula na lishe-TFNC, Mpango wa Kitaifa wa Kuthibiti Malaria-NMCP, USIAD, UNICEF, CDC, ICF International, Nutrition International, Royal Norwegian Embassy, DFID, GIZ, PSI, LHCR, GOT, Global Affairs Canada, United Kingdom FCDO, Irish Aid, German (KFW/GIZ), PSI

# Utekelezaji wa Utafiti (TDHS/MIS 2021-22)



## 01 Sampuli:

- Maeneo ya mjini - EA-211
- Maeneo ya vijijini - EA-418
- Jumla ya EA Tanzania-629
- Kila EA itakuwa na kaya 26
- Jumla ya kaya zitakazohojiwa Tanzania - 16,354

## 02 Mafunzo na Zoezi Halisi la Kuorodhesha Kaya:




Zoezi la kuorodhesha kaya lilianza na mafunzo ya Wadadisi na Wasimamizi yaliyofanyika mwezi Agosti 2021 jijini Dodoma yakijumuisha washiriki 80. Zoezi la kuorodhesha kaya lilianza rasmi tarehe 30 Agosti 2021 hadi tarehe 7 Oktoba 2021. Jumla ya maeneo ya kufanyia Utafiti (EAs) 629 yaliorodheshwa. kazi ya kuorodhesha kaya imekamiliwa kwa asilimia 100.

## 03 Mafunzo na Utafiti wa Majaribio:

Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa TDHS/MIS wa mwaka 2021-22 ni Kufanya Mafunzo na Majaribio ya Vifaa vya Utafiti ambapo kazi hii ilianza kutekelezwa tangu 26 Septemba 2021. Kazi kubwa inayofanyika katika hatua hii ni kupitia nyenzo zote za utafiti, kuboresha na kufanyia majaribio nyenzo hizo ikiwemo Madodoso ya Utafiti pamoja na Mfumo wa Kukusanyia Taarifa.

**MAFUNZO YA WASHIRIKI WA UTAFITI WA MAJARIBIO WA AFYA YA  
UZAZI NA MTOTO NA VIASHIRIA VYA MALARIA TANZANIA WA  
MWAKA 2021-22 (TDHS-MIS 2021/22)**

## Mafunzo ya Nadharia

-  Mafunzo ya Madodoso
-  Mafunzo ya Vipimo vya Mwili na Hali ya Vitamini na Madini Mwilini
-  Mafunzo na Majaribio ya Nyenzo za Utafiti







# Mafunzo ya Vitendo








# TAARIFA ZITAKAZOKUSANYWA

Utafiti wa DHS-MIS 2021-22 utakusanya takwimu katika ngazi ya kaya (households) kwa dhumuni la kuwezesha upatikanaji wa takwimu sahihi na zenye ubora kuhusiana na taarifa za msingi za kaya na jamii.

Taarifa hizi zitakusanywa kwa kutumia madodoso kama yalivyoainishwa hapa chini;



Dodoso la  
Kaya



Dodoso la  
Mwanamke



Dodoso la  
Mwanaume



Dodoso la  
Vipimo

# MADODOSO



DEMOGRAPHIC AND HEALTH SURVEY  
MODEL HOUSEHOLD QUESTIONNAIRE

FORMATTING DATE: 17 May 2020  
ENGLISH LANGUAGE: 17 May 2020

[NAME OF COUNTRY]  
[NAME OF ORGANIZATION]

**IDENTIFICATION (I)**

PLACE NAME \_\_\_\_\_

NAME OF HOUSEHOLD HEAD \_\_\_\_\_

CLUSTER NUMBER \_\_\_\_\_

HOUSEHOLD NUMBER \_\_\_\_\_

HOUSEHOLD SELECTED FOR MHS SURVEY? (1=YES, 2=NO) \_\_\_\_\_

HOUSEHOLD SELECTED FOR DHS? (1=YES, 2=NO) \_\_\_\_\_

**INTERVIEW VISITS**

	1	2	3	FINAL VISIT
DATE				DAY _____ MONTH _____ YEAR _____
INTERVIEWER'S NAME				INT. NO. _____
RESULT*				RESULT* _____
NEXT VISIT: DATE				
TIME				
*RESULT CODES:				TOTAL NUMBER OF VISITS _____
1 COMPLETED				TOTAL PERSONS IN HOUSEHOLD _____
2 NO HOUSEHOLD MEMBER AT HOME OR NO COMPETENT RESPONDENT AT HOME AT TIME OF VISIT				TOTAL ELIGIBLE WOMEN _____
3 ENTIRE HOUSEHOLD ABSENT FOR EXTENDED PERIOD OF TIME				TOTAL ELIGIBLE MEN _____
4 POSTPONED				LINE NO. OF RESPONDENT TO HOUSEHOLD QUESTIONNAIRE _____
5 REFUSED				
6 DWELLING VACANT OR ADDRESS NOT A DWELLING				
7 DWELLING DESTROYED				
8 DWELLING NOT FOUND				
9 OTHER _____ (SPECIFY)				
LANGUAGE OF QUESTIONNAIRE: 0 2	LANGUAGE OF INTERVIEW: 0 2	NATIVE LANGUAGE OF RESPONDENT: _____	TRANSLATOR USED (YES = 1, NO = 2) _____	
LANGUAGE OF QUESTIONNAIRE: <b>ENGLISH</b>		**LANGUAGE CODES: 01 ENGLISH 02 KISWAHILI 03 KISWAHILI 04 LANGUAGE 4 05 LANGUAGE 5 06 LANGUAGE 6		
TEAM _____	TEAM SUPERVISOR _____	CARI SUPERVISOR _____		
NUMBER _____	NAME _____ NUMBER _____	NAME _____ NUMBER _____		

Note: Questions with highlighting in the question number column may be deleted in some circumstances (see footnotes). Brackets [ ] indicate items that should be adapted on a country-specific basis.



01

## Dodoso la Kaya

Dodoso hili litatupatia taarifa zinazohusiana na Umri, Jinsia, Ulemavu, Elimu, Uhai wa wazazi kwa watoto wenye umri chini ya miaka 18, upatikanaji wa maji ya kunywa na matumizi mengine, umiliki wa mali za kudumu za kaya, sakafu ya nyumba, Aina ya paa la nyumba, Umiliki na matumizi ya vyandarua, vyoo na usafi wa mazingira, nishati za kuangazia na kupikia. Pia, litatuwezesha kuwatambua wanawake, wanaume na watoto wanaostahili kuhojiwa madodoso binafsi kupitia umri unaostahili kwa mahojiano binafsi na vipimo husika.



# MADODOSO

## 2. Dodoso Binafsi

Dodoso hili linakusanya taarifa za wanaume wenye umri kuanzia miaka 15-59.

Taarifa za umri na elimu, Afya ya Uzazi, Uzazi wa Mpango, Ndoa na tendo la kujamiiana, Upendeleo wa idadi ya watoto, Ajira na majukumu ya kijinsia, Uelewa juu ya VVU na UKIMWI, Taarifa zingine kuhusu afya, Mtazamo dhidi ya ukeketaji na Ufahamu na Imani kuhusu malaria.

### 2.1 Dodoso la Mwanaume



### 2.2 Mwanamke

Dodoso hili linakusanya taarifa za wanawake wenye umri kuanzia miaka 15-49.

Taarifa hizo zinajumuisha; Historia ya uzazi, Uzazi wa mpango, Huduma za afya wakati wa ujauzito na baada ya kujifungua, unyonyeshaji na lishe ya mtoto, Chanjo kwa watoto chini ya miaka 5, Ndoa na tendo la kujamiiana, Upendeleo wa idadi ya watoto, Uelewa juu ya VVU na UKIMWI, Ukatili dhidi wa wanawake majumbani, Ukeketaji kwa wanawake, Taarifa zingine kuhusu afya, na Ufahamu na Imani kuhusu malaria, Malezi na makuzi ya Watoto, Vifo vya watu wazima na vifo vitikanavyo na uzazi.

### 2.2 Dodoso la Mwanamke

### 3. DODOSO LA VIPIMO



Vipimo vya uzito, urefu, malaria na anemia kwa watoto chini ya miaka 5 na wanawake wenye umri wa miaka 15-49




Kipimo cha mkojo kwa wanawake wenye umri wa miaka 15-49 ili kutambua madini ya iodine, Upimaji wa shinikizo la damu kwa wanawake wenye umri wa miaka 15-49 na wanaume wenye umri wa miaka 15-59.





# Taarifa Nyingine ni Pamoja na;



01

Hali ya lishe ya akina mama wenye umri wa Miaka 15 hadi 49 na watoto chini ya umri wa miaka 5

02

Viwango vya vitamini na madini mwilini, miongoni mwa akina mama wenye umri wa miaka 15 hadi 49 na watoto chini ya miaka 5

03

Kipimo cha Kiwango cha Damu

04

Vipimo vya ugonjwa wa Malaria

05

Uongezaji wa Virutubishi katika vyakula

06

Hali ya lishe miongoni mwa wanaume wenye umri wa miaka 15 hadi 59

07

Shinikizo la damu

# Hali ya lishe ya akina mama wenye umri wa Miaka 15 hadi 49 na watoto chini ya umri wa miaka 5



Utafiti huu unajumuisha viashiria ambavyo vitaonyesha hali ya lishe miongoni mwa akina mama wenye umri wa miaka 15 hadi 49, watoto chini ya miaka 5 pamoja na wanaume wenye umri wa miaka 15 hadi 59.

Viashiria hivi vinakusanywa na madodoso mbalimbali, kama vile dodoso la kaya, dodoso la mwanamke na dodoso la vipimo. Kwa ujumla, utafiti huu utatoa picha halisi ya hali ya lishe katika ngazi Mkoa, Kanda na Kitaifa, na pia ulinganifu baina ya maeneo ya mijini na vijijini.



TAARIFA ZITAKAZOKUSANYWA



# Viwango vya vitamini na madini mwilini, miongoni mwa akina mama wenye umri wa miaka 15 hadi 49 na watoto chini ya miaka 5



Ukilinganisha na tafiti zilizopita, utafiti huu utahusisha viashiria vingi vinavyopima viwango vya vitamini na madini mwilini miongoni mwa wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 49 na pia watoto chini ya miaka mitano.

Viashiria vitakavyopimwa ni pamoja na Viwango vya

- madini chuma,
- asidi ya foliki,
- vitamini B12,
- vitamini A
- na madinijoto.



TAARIFA ZITAKAZOKUSANYWA

# Kipimo cha Kiwango cha Damu



Tafiti nyingi hapa nchini zimeonyesha kuwa tatizo la upungufu wa damu miongoni mwa wanawake na watoto bado ni kubwa, hivyo utafiti huu pia utakusanya takwimu zinazohusu viwango vya damu miongoni mwa akina mama na watoto; ili kutambua ukubwa wa tatizo hili katika maeneo yote nchini zitakazoweza kupanga afua mbalimbali za kulitatua.



**TAARIFA ZITAKAZOKUSANYWA**

# Vipimo vya ugonjwa wa Malaria



Utafiti huu utahusisha vipimo vya malaria miongoni mwa wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 49 na watoto wenye umri wa miezi 6 hadi 59. Vipimo vya malaria vitafanyika kupitia vipimo vya muda mfupi (mRDT).



TAARIFA ZITAKAZOKUSANYWA



# Uongezaji wa Virutubishi katika vyakula



Utafiti huu pia utahusisha vipimo vya kubaini hali ya virutubishi katika vyakula vinavyoliwa katika kaya.

Kwa kaya zitakazochaguliwa kushiriki, sampuli za unga wa mahindi, unga wa ngano, mafuta ya kupikia na chumvi zitakusanywa na kupelekwa maabara ya Taasisi ya Chakula na Lishe ili kupima viwango vya virutubishi vilivyomo.



TAARIFA ZITAKAZOKUSANYWA

# Hali ya lishe miongoni mwa wanaume wenye umri wa miaka 15 hadi 59



Utafiti huu utakusanya taarifa za wanaume wenye umri wa miaka 15 hadi 59, ambapo pamoja na viashiria vingine watapimwa urefu na uzito, pamoja na vipimo vya shinikizo la damu. Aidha, wanawake pia watapimwa shinikizo la damu kama moja ya kiashiria cha magonjwa yasiyo ya kuambukiza.



TAARIFA ZITAKAZOKUSANYWA

# Shinikizo la Damu



Aidha, utafiti huu utahusisha upimwaji wa shinikizo la damu kwa wanawake na wanaume watakoachaguliwa kushiriki. Vipimo vya shinikizo la damu ni moja ya kiashiria cha magonjwa yasiyo yakuambukiza.



TAARIFA ZITAKAZOKUSANYWA



# Afya ya Uzazi na Hali ya Uzazi

Utafiti huu utakusanya taarifa za msingi kuhusiana na Afya ya Uzazi na Mtoto, Viashiria vya Malaria na Lishe



TAARIFA ZITAKAZOKUSANYWA



## Ukatili wa kijinsia

Utafiti huu Utakusanya pia taarifa zinazohusiana na Ukatili wa Kijinsia katika maeneo Kisaikolojia, Kimwili, Kiafya, Kingono na Kiuchumi.

TDHS/MIS 2021-22



TAARIFA ZITAKAZOKUSANYWA





# MALARIA

## UFAHAMU NA IMANI KUHUSU MALARIA

Malaria ni ugonjwa unaoweza kuzuilika. Kuhakikisha kwamba watu wanafahamu namna ya kujikinga na kuzikinga familia zao dhidi ya malaria ni jambo muhimu katika kupambana na ugonjwa huu. Hivyo, taarifa, elimu na kuhamasisha mabadiliko ya mitazamo kuhusu malaria ni sehemu ya mkakati wa programu ya kitaifa ya kupambana na malaria.

Sote tunaelewa jukumu la kupambana na ugonjwa hatari wa malaria linahitaji nguvu na juhudi za pamoja kati ya wadau, Serikali na jamii kwa ujumla. Ikumbukwe kuwa nguvu na juhudi hizi za kupambana na ugonjwa wa malaria zinaanzia kwa mtu mmoja mmoja na kisha familia na jamii kwa ujumla. Hivyo basi, uwepo wa kipengele kinachohusu Ufahamu na Imani kuhusu Malaria katika Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2021-22 kutasaidia kupima uelewa kuhusu malaria na Imani potofu kuhusu ugonjwa wa Malaria. Utafiti huu umeweka maswali machache yenye lengo la kupima uelewa wa wananchi kuhusu ufahamu na imani kuhusu malaria. Maswali haya ya lengo la kutaka kujua iwapo;

- Wananchi Wameona Au Kusikia Ujumbe Kuhusu Kudhibiti Malaria Pamoja Na Vyanzo Vya Taarifa Hizo
- Wameona Au Kusikia Ujumbe Kuhusu Matibabu ya Malaria
- Wananchi Wanafahamu Dalili Za Malaria
- Ufahamu Wa Njia Za Kudhibiti Malaria
- Taarifa Za Mitazamo Kuhusu Malaria Hii Ikiwa Na Lengo La Kufahamu Iwapo Wanananchi Au Familia Inaweza Kumkinga Mtoto Dhidi Ya Malaria, Inaweza Kuhakikisha Watoto Wanalala Katika Chandarua Kila Siku, Inaweza Kutundika Chandarua Kwa Urahisi Kwa Ajili Ya Watoto Wao, na Inafahamu Umuhimu Wa Kulala Kwenye Chandarua Kila Siku.





# Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (Mb.)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO




Mchapa Kazi



KARIBU SANA



Kiongozi Mzalendo



Lishe Bora



Huduma Bora za Afya



Malazi Bora/Salama



Upendo/Huruma

TDHS/MIS 2021-22

19 OKTOBA 2021